# KCPE 2010

# KISWAHILI

## SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 40**

### SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali

### JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**

   **JINA LAKO**

   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu
9. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwa kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

   **MFANO**

   Katika kijitabu cha maswali:

   21. Tunakimbiana maana yake ni:
   A. Tunaogopana B. Tunahepana C. Tunasaidiana D. Tunachukiana

   Jibu sahihi ni **B**

   **Katika karatasi ya majibu**

   1 [A] [B] [C] [D] 11 [A] [B] [C] [D] 21 [A] ■ [C] [D] 31 [A] [B] [C] [D] 41 [A] [B] [C] [D]

   Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 21, kisanduku chenye herufi **B** ndicho kilichochorwa kistari

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

*© High Flyer Series, 2011* *Tel: 0722 – 81 95 95*

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Nilikimbia kadiri ___1___nikiacha ___2___ya jasho kudondoka kipajini. Sikujua kilichonipeleka ___3___humo. Daima babu yangu alikuwa ___4___dhidi ya kucheza karibu na mabaki ya nyumba zilizobomoka. ___5___niliyapuuza maneno yake. Sasa ___6___na hatari ya kuwa kitoweo ___7___mnyama ___8___.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | ningeweza | nilivyoweza | niliweza | niliyoweza |

**Jibu sahihi (B)** nilivyoweza.
Maelezo: Kiambishi (li) cha wakati uliopita kimetumika mwanzoni hatuosemi kadri niliweza wala niliyoweza.

2. matone | michirizi | mitiririko | mafunda

**Jibu sahihi (B)** michirizi
Maelezo: Matone ni ya mvua, mitiririko ni ya maji, vilevile mafunda yaweza yakawa ya maji, uji au sharubati.

3. kambini | handakini | mashambani | magofuni

**Jibu sahihi (D)** magofuni
Maelezo: Magofu ni mabaki ya kitu kilichobomoka kama vile nyumba za kale kama ilivyo kwenye mtungo.

4. amenishauri | ameniambia | amenikanya | ameniarifu

**Jibu sahihi (C)** amenikanya
Maelezo: Tunashauri, tunaambia au kuarifu kuhusu jambo lakini tunaonya dhidi ya hatari. Onya ni sawa na kanya.

5. Hata hivyo | Hata kama | Ingawa | Ijapokuwa

**Jibu sahihi (A)** Hata hivyo
Maelezo: Kiunganishi hiki hutumika kuonyesha ukanusho wa onyo. Yaani kando na kukanywa alipuuzilia mbali.

6. nitakabiliwa | nimekabiliwa | nilikabiliwa | nikabiliwa

**Jibu sahihi (B)** nimekabiliwa
Maelezo: Kutokana na matumizi ya kielezi (sasa) kinaonyesha muda ulipo: Siyo zamani wala baadaye.

7. na | ya | la | cha

**Jibu sahihi (D)** cha
Maelezo: Moja kwa moja mwanafunzi sharti aelewe ngeli ya nomino kitoweo ambayo ni (ki-vi) na unganifu ni 'cha'.

8. huyu | huyo | hii | hiyo

**Jibu sahihi (B)** huyo
Maelezo: viashiria hutegemea umbali kati ya vitu au watu husika huyu inamaanа anamuona myama huyo yawezekana anaaminika kuwa humo magofuni.

Kitendo cha ___9___ watoto kinapingwa na wanajamii ___10___. Wazo la kuwathamini watoto wa jinsia moja ___11___ nyingine ___12___ kukomeshwa. Mtoto ___13___ akipewa fursa bila shaka anaweza ___14___ mengi. Watoto basi wanahimizwa kutumia vipawa ___15___ ipasavyo.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 9. | kuwanyima | kuwapendelea | kuwanyakua | kuwabagua |

**Jibu sahihi (D)** kuwabagua
Maelezo: Kulingana na mtungo kubagua lina uzito kuliko kupendelea kwa sababu wanajadili jinsi sio makundi.

10. nyingi wengi wowote zozote
**Jibu sahihi (B)** wengi
Maelezo: Matumizi ya vivumishi vya pekee hutegemea muktadha wa sentensi.

11. kuliko kama kwa badala
**Jibu sahihi (A)** kuliko
Maelezo: Tunapolinganisha vitu viwili kwa ubora au udhaifu kiunganisha kuliko huwa mwafaka.

12. lilipaswa litapaswa linapaswa limepaswa
**Jibu sahihi (C)** linapaswa
Maelezo: Lazima mtahiniwa azingatie kiambishi cha wakati kifaacho kulingana na muktadha wa kifungu. Huu ni mjadala wala si kisa hivyo ni wakati uliopo (na).

13. mwingine yoyote yeyote pengine
**Jibu sahihi (C)** yeyote
Maelezo: Vilevile hapa mwanafunzi alitarajiwa kutumia kivumishi cha pekee mwafaka kulingana na ngeli ya nomino (mtoto)

14. kutekelezea kutekeleza kuelekėza kuelekezea
**Jibu sahihi (B)** kutekeleza
Maelezo: Mtego ulikuwa usahihi wa sarufi katika neno.

15. vyao zao vyenu zenu
**Jibu sahihi (A)** vyao
Maelezo: Ni vyema kuelewa mwendelezo wa ngeli kupitia nomino husika tunasema vipawa vyao ki-vi.

**Kutoka swali la 16 mpaka 30. Chagua jibu lililo sahihi.**

16. Chagua sentensi sahihi kisarufi.
   A. Msichana amenunua rinda nyingine nyeusi.
   B. Msichana amenunua rinda nyingine jeusi.
   C. Msichana amenunua rinda ingine nyeusi.
   D. Msichana amenunua rinda lingine jeusi.

   **Jibu (D)**
   **Maelezo:** Maneno yaliyo katika ngeli ya LI-YA, pamoja na- ingine huchukua 'JI' hivyo kulikuwa na utata kati ya jingine na lingine ingawaje (D) lilikaribia uwiano wa ngeli.

17. Chagua wingi wa sentensi hii:
   Ua ulizungushiwa waya.
   A. Maua yalizungushiwa waya.
   B. Maua yalizungushiwa nyaya.
   C. Nyua zilizungushiwa waya.
   D. Nyua zilizungushiwa nyaya.

   **Jibu sahihi (D)** Nyua zilizungushiwa nyaya.
   **Maelezo:** Ua ulizungushiwa .... (U-zi) wingi wa ua nyua
   - Ua lilizungushiwa .... (Li-Ya) wingi wa ua – maua.

18. Chagua kundi lenye vielezi pekee.
   A. Jabali, shujaa, mkakamavu, msomi.
   B. Mweupe, mdogo, membo, mnene.
   C. Ovyo, ghafla, kisiri, kwa gari.
   D. Omba, inua, osha, funga.

   **Jibu sahihi (C)**
   Maelezo: (A) ni nomino dhahania
   (B) vivumishi sifa (D) ni vitenzi

19. Nomino dhahania kutokana na kivumishi 'bora' ni:
   A. boreka B. uboreshaji
   C. kuboreka D. boresha

   **Jibu sahihi (B)** uboreshaji
   Maelezo: Nomino dhahania hujumuisha vitu vya kufikirika tu visivyoonekana wala kugusika hivyo bora itakuwa uboreshaji mengine ni hali ya kunyambua.

20. Chagua kiwakilishi katika sentensi hii:
   Wao hucheka hadi wakalia.
   A. wao B. wakalia
   C. hucheka D. hadi

   **Jibu sahihi (A)** wao

Maelezo: Viwakilishi hutumika badala ya nomino, hivyo basi neno wao linasimamia au kuwakiliwa watu fulani cheka ni kitenzi, vilevile lia, hadi ni kiunganishi.

21. Buibui ni kwa utando, ________ni kwa mchwa.
A. kichuguu B. kizimba
C. tundu D. mchangani
**Jibu sahihi (A)** kichuguu
Maelezo: Mwanafunzi alitarajiwa kujua makao mbalimbali. Kizimba ni cha kuku, tundu vilevile ni kwa ndege na mchangani ni jongoo miongoni mwa vimelea wengine.

22. Jua kuwa mtikati ni wakati wa:
A. mchana B. macheo
C. alasiri D. adhuhuri
**Jibu sahihi (D)** adhuhuri
Maelezo: Msamiati wa wakati jua la mtikati ni lile la adhuhuri pia huitwa la utosi.

23. Kamilisha: Matunda yamejaa sokoni ______.
A. chepechepe B. pomoni
C. nomi D. tiki
**Jibu sahihi (C)** nomi
Maelezo: Tanakali za sauti; tunalowa chepechepe, maji hujaa pomoni, mtu huchoka tiki nayo matunda hujaa kocho kocho au nomi yaani kwa wingi.

24. Chagua neno lisiloafikiana na mengine.
A. kupe B. mende
C. utitiri D. kunguni
**Jibu sahihi (B)** mende
Maelezo: Kupe, utitiri na kunguni ni vimelea wanao nyonya au kufyonza damu ya wanyama, mende hula mabaki ya vyakula na karatasi.

25. Meno hushikiliwa na nyama zinazoitwa:
A. taya B. shavu
C. kaakaa D. ufizi
**Jibu sahihi (D)** ufizi
Maelezo: Msamiati wa sehemu za mwili: taya ni mfupa unaoshikilia meno, shavu sehemu ya uso iliyo kushoto na kulia chini ya jicho. Kaakaa sehemu ya juu ya kinywa iliyo nyuma ya meno ya mbele.

26. Mtoto wa umbu huitwa:
A. mpwa B. mkoi
C. ndugu D. binamu
**Jibu sahihi (A)** mpwa
Maelezo: Msamiati wa ukoo. Binamu na mkoi ni sawa watoto wa shangazi au amu. Ndugu watoto waliozaliwa pamoja na mama.

27. Chagua kihusishi katika sentensi hii.
Najua tofauti baina ya mandarin na mandhari.
A. najua B. na mandhari
C. tofauti D. baina ya
**Jibu sahihi (D)** baina ya
Maelezo: Kiunganishi kati ya vitu viwili au watu wawili.

28. Geuza katika kauli ya taarifa: Baba aliwaambia wanawe, "Viwekeni vyumba vyenu safi kila siku."
A. Baba aliwaambia wanawe kuwa anataka waviweke vyumba vyao safi kila siku.
B. Baba aliwaambia wanawe kuwa angetaka waviweke vyumba vyao safi siku zote.
C. Baba aliwaamuru wanawe kuviweka vyumba vyao safi kila siku.
D. Baba aliwaambia wanawe kuwa yeye hutaka waviweke vyumba vyao safi kila siku.
**Jibu sahihi (C)**
Maelezo: Sentensi inatoa dhana ya amri hivyo basi wanawe hawakuwa na hiari ila kutii amri.

29. Chagua sentensi iliyo katika wakati uliopo hali isiyodhihirika.
A. Mimi hupika chakula.
B. Mimi nimepika chakula.
C. Mimi ninapika chakula.
D. Mimi napika chakula.
**Jibu sahihi (D)** mimi napika chakula
Maelezo: Mwanafunzi aelewe viambishi vya nyakati mbalimbali.

30. Chagua sentensi iliyoakifiswa vyema.
A. Ah! Umeanguka? Pole sana.
B. Ah, Umeanguka, Pole sana!
C. Ah, Umeanguka? pole sana.
D. Ah! Umeangua. Pole sana
**Jibu sahihi (A)**
Maelezo: Neno au sentensi yoyote iliyo na kihisishi lazima ishara ifuate kisha mengine hivyo (D) imekosa kiulizi (?) ambapo si sahihi. Katika kitengo cha ufahamu maswali huwa mseto kulingana na maudhui ya mwandishi hivyo majibu hubaini msomaji.

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 – 40.**

"Mgeni mheshimiwa, Daktari Busara, Mwalimu wetu, walimu, wanafunzi wenzangu, hamjambo! Kama mlivyotajiwa, mimi ni Kiranja Mkuu wa shule hii. Kwa niaba ya wanafunzi wa darasa la nane ningependa kuchukua fursa hii kuwashukuru walimu wetu kwa kutuletea mhadhiri ambaye ametupa mawaidha ya kutufaa. Bila shaka tukiyatilia maanani yote aliyoyanena yatatujenga maishani.

Mhadhiri ametukumbusha kuhusu umuhimu wa nidhamu. Ametilia mkazo matendo ya heshima na utiifu. Ametuhimiza kuyachuja mema na mabaya na kuzifuata kanuni zote muhimu maishani. Aidha ametuhimiza tutende mambo kwa wakati ufaao. Amesisitiza pia kuwa, tukifanya lolote tulitende kwa hadhari, mahali pafaapo. Yatupasa tuepuke njia zitakazotutumbukiza gizani.

Daktari Busara ametuzungumzia kuhusu mwingiliano mbaya kati ya marafiki shuleni na hata nyumbani. Ni muhimu kuyaepuka makundi yanayoshinikiza utandaji maovu. Tuhimizane kusoma katika makundi na kubadilishana mawazo bora. Amesema kuwa michezo ni muhimu kwani ina faida nyingi. Miongoni mwa faida hizo ni kuijenga miili na kuchangamsha akili. Hata hivyo, amesisitiza tena kuwa, kila jambo liwe na kipimo. Kucheza sana bila kusoma, kutayaathiri matokeo ya mitihani.

Bwana Busara amesema kuwa, maisha ya kesho hujengwa na maisha ya leo. Ni vyema kujiuliza, " kweli nimejenga nini leo? Je, nimekuwa nikijipakatia mikono siku hizo zote, nikijua kuwa muda upo na hapana haja ya kujisaga sana na vitabu?" Jamani wenzangu, tuamke sote kwa pamoja kama tulivyoshauriwa. Tusome kwa bidii kama mchwa wafanyavyo kazi zao. Tusitegemee kubebwa na wazazi, ndugu na marafiki. Tukumbuke kuwa, mtegemea cha nduguye....."

Nimefurahi mhadhiri aliposema kuwa, miaka kadhaa ijayo huenda tukajikuta kuwa viongozi. Viongozi wa kesho hujengwa leo. Nikajiuliza tena, "mimi nitaweza hata kuwa mhadhiri kama yeye?" Alipoendelea kusema kuwa maisha ya uzeeni huanzia utotoni, nilijua kuwa, huo ndio uhalisia wa mambo. Jinsi tunavyosoma sasa ndivyo tutakavyojiokoa kesho. Tukiuendekeza ugoigoi hatutafua dafu abadan! Tukumbuke tukilima pantosha, tutavuna pankwisha. Tuamke! Tusome kwa nia moja ya kujiimarisha maishani.

Mhadhiri ametuhimiza tuwe na malengo. Tujue tunataka nini maishani. Tuibuni mikakati ya kukipata kile tukitakacho. Ametuambia pia kuwa, mumu humu darasani, mtatoka madaktari, walimu, wahandisi na hata matopasi! Sasa uteuzi ni wetu. Utahisije kujikuta duni kazini, ukiwa na mwenzako mliyesoma pamoja katika mazingira sawa, sasa ndiye mkurungenzi wako? Tusome sote tuimarike, tupite kwenda shule bora za sekondari na huko uzi uwe ule ule kama tulivyoshauriwa. Tukaze kamba hadi chuo kikuu, tutakapokutana na Daktari Busara. Inawezekana! Muda ni huu! Tutie bidii.

Mimi nimepata mwamko. Kuanzia leo sitafikiria kuwa mchuuzi kama wazazi wangu. La! hasha! Ingawa kazi ni kazi na uchuuzi huo umenipa riziki tangu utotoni, sasa nataka nisome sana hatimaye niwe mhandisi wa kuunda hata ndege.

Jamani, furaha iliyoje hiyo kama sote tutajikuta katika baadhi ya nyadhifa na kazi bora zilizotajwa? Tutafanyaje tupige hatua hizo? Tujifunge vibwebwe kwani mchumia juani hulia kivulini.

Namalizia kwa kuwashukuru tena kwa kunisikiliza na kuzidi kumshukuru mhadhiri wetu wa leo na walimu. Nanyi wenzangu, tumepewa motisha leo. Natumai tumeamka kutoka katika usingizi wetu wa pono. Tuahidi kukazana kama nyuki. Asanteni."

31. Kwa mujibu wa aya ya pili nidhamu huhusu mambo yafuatayo ila:
   A. kuogopa mabaya yanapotujia
   B. kutenda mambo mema kwa tahadhari
   C. kutenda mambo yanayokubalika
   D. kuwa mahali pafaapo ikihitajika.

   **Jibu sahihi (A)**
   Maelezo: Mhadhiri anawahimiza kuyachuja mema na mabaya wala si kuyaogopa.

32. Maana ya 'Zitakazotumbukiza gizani" ni:
   A. zitakazotuathiri
   B. zitakazotupotosha
   C. zitakazotukosesha hadhari
   D. zitakazotukosesha mwanga.

   **Jibu sahihi (B)**
   Maelezo: Kutumbukia gizani ni kupoteza mwelekeo sawa na kupotoka.

33. Kulingana na kifungu, umuhimu wa michezo ni:
   A. kuhimiza mwingiliano wa makundi
   B. kuhimiza kufanya mambo kwa kipimo
   C. kutuliza akili na kuimarisha miili
   D. huleta tahadhari na kuimarisha matokeo.

   **Jibu sahihi (C)**
   Maelezo: Michezo husaidia kuijenga mili na kuchangamsha akili; akili kichangamka inapata utulivu.

34. Maisha ya kesho hujengwa na maisha ya leo inamaanisha:
   A. ukitaka kuishi vyema baadaye sharti uweke msingi sasa
   B. maisha mema ya baadaye sharti yawekewe msingi
   C. maisha ya leo ni sawa na maisha ya kesho
   D. ukitaka kuishi kesho lazima uishi vizuri leo.

   **Jibu sahihi (C)**

   Maelezo: Mwandishi anamithilisha kujenga na ile hali ya ujenzi ina maana kuwa mjengo wowote sharti uwe na msingi.

35. Maana ya nikijipakatia mikono ni:
   A. Kutofanya chochote
   B. Kutotazamia chochote
   C. Kubaki ukishangaa
   D. Kukaa ukihuzunika

   **Jibu sahihi (A)** semi

   Maelezo: Mapambo ya lugha. Kujipakatia mikono ni semi iliyo na maana kukaa bure bila kufanya lolote zebea.

36. Kwa mujibu wa kifungu Tukilima pantosha tutavuna pankwisha ina maana:
   A. tukilima shamba dogo hatutapata mavuno mengi
   B. tukiridhika na kidogo hatutatamani vingi
   C. tukitosheka na shamba dogo hatutatafuta kubwa
   D. tukitia bidii kidogo tutapata mafanikio haba.

   **Jibu sahihi (D)** methali

   Maelezo: Ukipanda pantosha utavuna pankwisha, maana ya ndani ni kuwa ukitia bidii kidogo utafaidi kidogo bidii kubwa faida kubwa.

37. Kulingana na kifungu hiki, lengo kuu la kupata elimu ni:
   A. kujipatia sifa kubwa
   B. kujiimarisha na kuimarisha jamii
   C. kuweza kujiteulia mambo maishani
   D. kupata vyeo vikubwa na utajiri.

   **Jibu sahihi (C)**

   Maelezo: Mhadhiri anasisitiza kipawa na uwezo wa kuweza kujiamulia mambo bila kutegemea wala kuiga wengine.

38. Katika aya ya sita maoni ya mhadhiri ni kwamba:
   A. kusomea katika mazingira sawa huwahakikishia wanafunzi nafasi sawa baadaye
   B. wanafunzi waliosomea katika mazingira sawa wana hakikisho la kuwa na mitazamo sawa
   C. wanafunzi waliosomea katika mazingira sawa wanatakiwa wajitofautishe kitaaluma
   D. kusomea katika mazingira sawa huwezi kujenga watu wa taaluma tofauti.

   **Jibu sahihi (D)**

   Maelezo: Maoni yake ni kuwa mazingira sawa yanaweza kutoa taaluma mbalimbali kulingana na malengo ya wasomi.

39. Mimi nimepata mwamko ina maana:
   A. Awali kiranja alikuwa hajui umuhimu wa elimu
   B. Awali kiranja hakuwa ameyawekea maisha yake malengo
   C. Awali kiranja hakuwa na malengo makubwa maishani
   D. Awali kiranja alikuwa hajui kazi nyingine.

   **Jibu sahihi (C)**

   Maelezo: Unapopata mwamko ina maana umefunguka macho na kuzidisha kiwango cha yale uliyoyadhania hapo awali.

40. Kwa mujibu wa kifungu, kupata baadhi ya nyadhifa na kazi bora kunahitaji:
   A. kuwa na tumaini na motisha
   B. kujitahidi kwa vyovyote vile
   C. kuamka kutoka usingizini
   D. kufanya kazi tangu utotoni

   **Jibu sahihi (B)**

   Maelezo: Kwa jumba mbadhiri amepigana na uzohali na malengo duni huko akiipa biddi na jitihada kipaumbele.

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.***

Bara la Africa lina takriban mataifa hamsini na manne. Kila taifa limetengwa na kubainishwa kwa mipaka yake ya kitaifa iliyopangwa kwa sababu za kisiasa zinazohusisha misingi ya utawala. Kutokana na mipaka hii, mataifa mengine ni madogo kama vile Rwanda na Burundi na mengine ni makubwa kama Tanzania, Kongo na Kameruni. Ifahamike kwamba ukubwa au udogo si hoja kwa taifa ikiwa linaweza kujisimamia. Bora tu pawe na serikali inayotekeleza majukumu yake.

Kawa ajili ya tofauti za kitaifa, yamkinika ingekuwa vigumu sana kwa utawala mmoja kuweza kumiliki na kudhibiti eneo lote la Africa mashariki na kati. Fikiria jinsi serikali moja inavyoweza kutawala kuanzia visiwa vya Lamu kule upwa wa pwani hadi kufikia Kameruni, upande wa Afrika Magharibi.

Kuna umuhimu wa kuweka mipaka ya kitaifa. Jambo la kwanza ni kurahisisha utawala. Kwayo serikali huweza kutekeleza miradi yake kwa urahisi katika eneo lake. Hali kadhalika, watu wanoishi katika eneo moja hujenga uhusiano wa karibu na kufahamiana vyema. Hali hii hukuza ushirikiano zaidi. Umuhimu mwingine hujikokeza kwa upande wa kujenga hisia za umoja miongoni mwa wote wanaoishi katika eneo moja. Umoja huu huwa na mvuto wa kidugu unaotia watu ari ya kutaka kujitambulisha kama raia wa sehemu moja. Bila hisia za umoja na udugu, kwa hakika haingewezekana kuwa na taifa madhubuti.

Mbali na mipaka,kuna tamaduni na mila za kiasili zinazozibainisha jamii mbalimbali. Tukiangazia upande wa vyakula itadhirika kuwa, vile vilivyozoeleka eneo moja ni tofauti na vyakula vya kawaida vya eneo lingine. Kwa mfano katika mataifa ya Africa Magharibi hasa Nigeria, chakula chao mahsusi huitwa 'foo foo'. Nchini Kenya ugali ndicho chakula cha muhimu miongoni mwa jamii nyingi. Waganda hupendelea 'matoke' zaidi. Mazoea yana taabu. Mtu huenda asitosheke na mapochopocho ya biriani na pilau mfululizo bila kuonja chakula chao asilia.

Mavazi pia ni mojawapo ya vitambulisho vya tamaduni za jamii mbalimbali. Mathalan Afrika Magharibi ni maarufu sana kwa mavazi yao ya aina ya vitenge vilivyotiwa nakshi na kushonwa kwa urnaridadi. Nyuzi za rangi ali ali hutumiwa kuongezea urembo wa vitenge kuthibitisha kwamba ukiviona vinaelea jua vimeundwa. Mavazi haya huvaliwa na wanaume na wanawake, tofauti zikijitokeza kwenye mitindo na mishono. La ziada, wanaume hukamilisha vazi lao kwa kuvaa kofia maalum. Wanawake nao hujifunga kitambaa kichwani kila mmoja kwa ufundi wake.

Kila taifa lina lugha yake maalum ambayo hujulikana na kutumiwa na raia wake wote kama lugha unganishi. Lugha hii teule hitwa lugha ya taifa na inatumika katika shughuli za serikali, biashara na mawasiliano ya kila siku miongoni mwa wanajamii.

Katika mataifa ya Kenya na Tanzania, Kiswahili kimetumiwa kwa miaka mingi kama lugha ya taifa. Kwa upande mwinginge, Luganda ndiyo lugha iliyopewa kipaumbele huko Uganda japo Kiswahili hutumiwa pia. Nchini Kongo kuna baadhi ya lugha teule za taifa zikiwemo Lingala na Kingwana.

Ni kweli kuwa nchi za kiafrika zina mengi yanofanana kama vile kuwa na historia ya kutawaliwa na wakoloni, mali ya asili kama vile machimbo ya migodi, sherehe za kitamaduni zikiwemo ndoa na posa. Hata hivyo ibainike kuwa kila jamii ina tamaduni zake mahsusi zinazoitofautisha na nyingine. Ni muhimu kujivunia tamaduni hizo kwani mwacha mila ni mtumwa.

41. Bara la Afrika lina takriban mataifa hamsini na manne inamaanisha:
   A. lina karibu mataifa hamsini na manne
   B. lina zaidi ya mataifa hamsini na manne
   C. lina mataifa hamsini na manne
   D. lina chini ya mataifa hamsini na manne.

**Jibu sahihi (A)**

Maelezo: Neno Takriban kulingana na kamusi linamaanisha hali ya kukaribiana kwa vitu, hali au idadi: karibu ya mataifa hamsini na manne.

42. Kulingana na taarifa, ubora wa taifa hupimwa kwa:
   A. utamaduni wake
   B. uwezo wa kujitegemea
   C. uwezo wa kuweka mipaka
   D. serikali yake.

**Jibu sahihi (D)**

Maelezo: Ni wazi kuwa serikali isiyotekeleza sera zake za utawala haiwezi ikawa madhubuti.

43. Mipaka ya Kitaifa:
   A. hutambulisha watawala
   B. huimarisha uzalendo
   C. huimarisha ubunifu
   D. hutambulisha utamaduni.

**Jibu sahihi (B)**

Maelezo: Aya ya tatu inatajia mshikamano na ushirikiano wa watu wa eneo moja hivi kuwa wanainua na kudumisha uzalendo.

44. "Bila hisia za umoja na udugu kwa hakika haingewezekana kuwa na taifa madhubuti." Methali inayoweza kujumuisha kauli hii ni:
   A. Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.
   B. Papo kwa papo kamba hukata jiwe.
   C. Kinga na kinga ndipo moto uwakapo.
   D. Udugu wa nazi hukutania chunguni.

**Jibu sahihi (C)**

Maelezo: Methali hii inaonyesha umoja na ushirikiano wa watu ukidumishwa maendeleo yatapatikana.

45. Kulingana na kifungu, kuishi katika eneo moja husababisha:
   A. kutegemeana na kupendana
   B. kutiana ari na kutambuana
   C. kujenga aifa na kuelewana
   D. kushirikiana na kufahamiana.

**Jibu sahihi (D)**

Maelezo: Tukizingatia kifungu katika aya ya tatu mshororo wa pili mwandishi ametanguliza kwa kuhusiana na kujuana.

46. Kulingana na kifungu, '<u>mazoea yana taabu</u>' inamaanisha:
   A. mtu akizoea biriani hatatamani vyakula vingine
   B. mtu akizoea chakula cha kienyeji hatatamani mapochopocho
   C. mtu hutamani chakula alichozoea kuliko kizuri alichoandaliwa
   D. mtu hutamani chakula mahsusi kuliko kizuri alichoandaliwa.

**Jibu sahihi (C)**

Maelezo: Kutokana na msemo mazoea ni bayana kuwa ni ile hali na kurudiarudia lolote ulifanyalo unashikwa na shauku.

47. Huko Afrika Magharibi vitenge vilivyonakshiwa:
   A. hupendelewa na wanawake wote
   B. hutofautisha wanawake na wanaume
   C. hupendelewa na wanajamii wote
   D. hutofautisha jamii moja na nyingine.

**Jibu sahihi (B)**

Maelezo: Katika ibara ya tano, tunaelezwa tofauti huwa kwenye mitindo na mishono kama vile kofia maalum na vitambaa.

48. Lugha unganishi:
   A. ni ile inayounganisha mataifa
   B. ni ile inayofahamika na kutumiwa na wote
   C. ni ile inayotumiwa katika biashara
   D. ni ile inayojumuisha watu wa jamii zote.

**Jibu sahihi (D)**

Maelezo: Jamii mbalimbali zina lugha zao asili ambazo hazieleweki na jamii nyingine lakini lugha ya taifa hutumiwa na jamii zote.

49. Kifungu kinasema kwamba Kiswahili kimetumika kama kitambulisho:
   A. Tanzania na Kenya
   B. Afrika Mashariki
   C. Kenya na Uganda
   D. Tanzania na Uganda

**Jibu sahihi (A)**

Maelezo: Uganda hutumia luganda huku ikieleweka wazi kuwa Uganda ni mojawapo ya nchi za Afrika Mashariki.

50. Kichwa kinachofaa zaidi taarifa hii ni:
   A. Mwacha mila ni mtumwa
   B. Tofauti kati ya Afrika Mashariki na Magharibi
   C. Vitambulisho vya jamii
   D. Vitambulisho vya tamaduni.

**Jibu sahihi (A)**

Maelezo: Mwandishi ametajia kuhusu Bara la Afrika kwa ujumla na amezingatia mengi kuhusu utamaduni wa jamii mbali mbali katika nchi tofauti kwa hivyo lengo lake ni tabia yaani mila na itikadi za kiafrika ambazo ni tamaduni hivyo basi methali hii ni mwafaka.